**Jiwe la kiroho la kujengea Namba 31.**

# UWEZA WANGU HUTIMILIKA KATIKA UDHAIFU WANGU.

*"Naye akaniambia, neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi,ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu* ***(IIWakorintho 12: 9-10)***

*Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu vidhaifu vya dunia ili aviabishe vyenye nguvu*. ***(I Wakorintho 1:27)***

Tunajaribu kutoa udhuru kwaajili ya madhaifu yetu. Tunapenda kuambiwa jinsi tulivyo watu bora..jinsi tulivyo watu wakubwa. Nafikiri ndiyo mojawapo ya mambo yaliyofanya Mungu anipe somo hili, ni kulitoa hilo nje kutoka kwenye fikira zetu.

Kuna mambo madogo ambayo tunaweza kufanya. Na hayo ndiyo tunayojia kanisani, **ni kutafuta** ***wapi tunamadhaifu, na hayo madhaifu ndiyo tunaweza kujifanya wenyewe kuwa bora zaidi kupitia hayo.kama tunakuja kanisani kwa lengo lingine lolote kuliko hili, ninawasiwasi hatutapata mengi kwa njia ya kuja kanisani. Lazima tuje kutafuta madhaifu yetu, kutafuta mahali petu mabaya na kujiona jinsi tulivyo watu wadogo sana na kuweka tumainini letu kwa mtu Fulani aliye imara sana***.

Kuna wengi wetu wanapenda kusifiwa au kufikiri kwamba hatujitoshelezi; na kwahiyo, tunafanya hilo liwe udhuru., " sina elimu; sina uwezo; siwezi kufanya hili; na kama utaendelea na hilo na kufanya hivyo, unaendelea kufanya kama hivyo, ndipo hutaweza kufanya kitu chochote.lakini kile kitu tunachopenda kukitolea udhuru, Mungu anatumia hichi na huo udhaifu umfanyie kazi yake. Unaona? Anatusibiri tuwe katika hali hiyo ili aweze kututumia. Tunatoa udhuru na kusema, vyema siwezi kufanya hilo, sina uwezo, siwezi kufanya hili, na Mungu anatumia huwo udhaifu kufanya kazi nao. Hiyo ni kweli.

Hiyo ndiyo sababu ya **kwanini alituchagua sisi, ni kwasababu tupo katika hali hiyo.**

***( I Wakorintho. 1: 26-29)***. Sasa, linasikika la kigeni, lakini baada ya dakika chache tu, tutapata sababu yake, kama Mungu akipenda.

Angalia inahitaji madhaifu na kukataliwa, na kwa udhahiri kabisa, kila mpenzi wa Mungu aliyeweza kuwepo kwenye mstari wa mbele kwaajili ya Mungu alikuwa wa kukataliwa. ***(Waamuzi. 6:11-24)***. Mtu aliyekataliwa, mtu aliyefikiri hajitoshelezi, mtu ambaye hakuwa na uwezo kabisa, ndipo huyo mtu yupo katika umbo ambalo Mungu anaweza kumtumia. Unaona?hiyo ni sahihi, wanapofikiri kana kwamba hawataweza, hawana kitu chochote, hapo

ndipo Mungu anaweza kuwashikilia na kufanya jambo Fulani nao. Unaona? Lakini tunapofikiri kwamba tunaweza, kisha Mungu hawezi kututumia sababu tunataka kulifanya hilo wenyewe.

Na kisha, kwa upande mwingine,tunapata haya mawazo na tunafikiri kwamba hatujitoshelezi, na hatutaki kulifanya hilo,basi kama tu tutasikiliza mwito wa Mungu, hicho ndicho kitu hasa Mungu anataka tukiendee, hiyo ndio hali anaitaka ili aweze kufanya kazi yake.

Pale tunapokuwa hatujitoshelezi wenyewe, basi ujue tupo katika hali ya kumleta Roho wa Mungu ***(II Wakorintho 20:1-23).*** Na ilimradi tunafikiri tunaweza kufanya kitu ujue hatuwezi kufanya kitu. Lakini pale tunapofika mahali ambapo tunajua hatuwezi kufanya chochote tutajihudhurisha wenyewe kwa Mungu na hapo yeye atafanya hilo. Hivyo kama ni sisi tunaojaribu kufanya kitu tutashindwa. Lakini kama tutajiachia wenyewe kwa Mungu ndipo Mungu hawezi kushindwa.

Kuna jambo moja tu ambalo Mungu hawezi kufanya, na nikushindwa. Anaweza kufanya kitu kingine chochote lakini sio kushindwa. yeye hawezi kushindwa.

Ili mradi tunajaribu kulifanya wenyewe na kutegemea uwezo wetu wenyewe, nini, hatutafanya kitu, lakini tunapofika mahali tunapojua hatufai kitu, hapo Mungu anaweza kututumia.

Kitu muhimu sana, moja ya jambo muhimu sana ambalo tunaweza kufanya….., sasa, kumbuka hili, ni hususan kwa ninyi vijana wahubiri, na washirika wa aina hiyo, kuna kitu kimoja ambacho tunatakiwa kukifahamu kama tunategemea kutimiza mapenzi ya Mungu maishani mwetu; ni kufahamu uwezo wa mawazo ya mwanadamu. Kama tunafika kwenye pointi ambayo tunafikiri tunaweza kufanya jambo wenyewe kwa kutumia ufahamu wetu, na uwezo wetu, tunapaswa kuondoa hayo mawazo na kuweka hicho kitu pembeni hivyo kwamba Mungu aweze kututumia.hiyo ni sahihi.

Na jiachilie kikamilifu! Hatuwezi kutumia uwezo wetu. Tunapaswa kujiachilia kikamilifu na kuja kwa Mungu, unapaswa kujitoa kwake kuanzia Nafsi, mwili na Roho. Kila kitu ulichonacho kiachie kwa Mungu ili aweze kufanya kazi yake ndani yako na ndani yangu.
***(I Wakorintho. 6:19-20)***

Sasa, hilo ni gumu; ninajua sababu siku zote tunataka kuchangia sehemu yetu kitu Fulani tunachokijua, unajua, kwamba tunataka kufanya hivyo, tunasema, sawa, ninajua inapaswa ifanyike hivi, lakini ili mradi unafanya hivyo, unakwenda kukosea, na Mungu kamwe hatatumia hiyo juhudi yako.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa ulimwengu leo: kuna uzoefu mwingi wa kutoka kwenye seminari, vitu vingi vilivyoletwa na elimu, mengi kutoka kwenye ushirika na mahusiono ya kidhehebu; tunategeme hayo kutoka mmoja kwa mwingine, tunategemea uwezo uliotoka kwa wanadamu.

Pale tunapotarajia, na kusema, huyu mtu ni mkubwa, huyu ni mtu mkubwa, ninaweka tumaini langu juu yake” hilo halimfurahishi Mungu unapofanya hivyo.tunapaswa kuweka tumaini letu

juu ya Mungu na Mungu pekee. ***(Methali 3:5-6).*** Hatupaswi kuweka tumaini letu kwa uwezo wetu wenyewe au kwa mtu yeyote. Tunapaswa kumtegemea mungu kikamilifu.

Sio uwezo, sijali yukoje, haitasaidia machoni pa Mungu. Mungu anatoa uwezo wetu wote kabla ya kufanikisha lengo lake kupitia sisi.kama anakitu chochote anachotaka tukifanye, na ili mradi tunajisikia kukifanya vizuri wenyewe ujue kamwe hatutaweza kutumiwa na Mungu.

Sikiliza Mtume Paulo kwa ***( I Wakorintho 2: 1-5),*** na *nilikuja kwenu katika*…….( ukubwa? Wanini?) wa *udhaifu, na kwa hofu na kwa matetemeko mengi*

Ungeweza kufikiria mtu, mfarisayo wa mafarisayo, mwalimu wa walimu, mtu aliyefunzwa tangu utotoni kwaajili ya huduma ya wenye elimu, watu mashuhuri na wenye akili sana, na aje kwenye daraja la watu kama wakorintho na aseme “ nilikuja kwenu na udhaifu,na kwa hofu kuu, na kwa matetemeko mengi” mtu aliyeweza kuugeuza ulimwengu ukawa juu chini.mmishenari mkuu ambaye hajawahi kuwepo, akiri kwamba alikuja kwao kwa unyonge, sio mtu mwenye elimu, bali kwa unyonge na hofu, aliweza kutoa ufahamu wake kwa njia ya mateso mengi na, ndiyo sababu hakuweza kutegemea uwezo wake.

Sababu yeye aliogopa, sio kwamba yeye alihofu kitu chochote; lakini aliogopa kwamba angeweza kumuudhi Mungu kwa namna fulani.kwamba angetumia uwezo wa kiungu na akauchanganya na vitu alivyojifunza. Aliwaambia wao hilo, sikuja kwenu na uzoefu wa hotuba nzuri za kibinadamu; sikuja kwenu na hofu ya namna hiyo.lakini nimekuja kwenu nikiwa sijui kitu ila Kristo pekee aliyesulubiwa’ ***( I Wakorintho 1: 18-25; Wagalatia. 6:14)***

“*Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa madhihirisho ya nguvu za Roho,”*

Msikilizeni huyu mtu ambaye alikuwa tishio alijishusha mwenyewe. Amina. Kama kunakitu chochote ambacho shule zetu zingekihitaji leo, kama kuna kitu makanisa yetu yangekihitaji leo**,** nikujishusha wenyewe, kutoka kwenye mawazo yao na uwezo wao .jishushe mwenyewe mbele za Mungu bila hivyo utajaribu kufanya kitu Fulani kilicho kwenye uwezo wako mwenyewe.

Natumaini hilo linaingia kwenye kilindi cha mioyo yetu. Na ujitambue kuwa unapaswa kuwa si chochote, asiyejua kabisa, sio mtu mkubwa lakini ambaye si chochote.inabidi uwe vumbi, inabidi ufike mahali unaweza kujiona kuwa wewe sio kitu. Na kamwe usipande kukidhidi hicho, kwa sababu punde utakapopanda na kukipita hicho unamdhidi Mungu. Inabidi ujishushe mwenyewe kuwa kama mavumbi na uendee njia ya Damaski ***(Matendo. 9: 1-21).*** Inakubidi ujitoe kwenye njia kuu.

“Mahubiri yangu” yeye alisema “*kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu bali kwa madhihirisho ya nguvu za Roho,”*Sasa angalia. Kulikuwa kuna nini kwa Paulo? kwanini msingekifanya hiki?

“*Kwamba imani yenu isiwe ya hekima ya kibinadamu bali iwe ndani ya Nguvu za Mungu”*

Ooooh, ni mhubiri wa namna gani! Alimtafuta Mungu naye akasema," Mungu Mimi nidhaifu na sijui namna ya kutenda. Ninakuomba wewe, Mungu, unifanye niwe mwenye nguvu, chukua manyonge yangu, na mambo haya yote, ili niweze kuwa mwenye nguvu."

Mungu akamjibu Paulo na Kusema, "Paulo, Uweza wangu hutimilika katika madhaifu yako**"(*IIWakorintho. 12:9-10)***

Kisha Paulo akasema"kama nikiwa dhaifu ndipo ninapokuwa na Nguvu" ndiyo akasema basi nayatukuza manyonge yangu na madhaifu yangu. Ninamshukuru Mungu kwamba yote yametoka nje ya mwili wangu, na ninapotoa kila kitu mwilini mwangu, ndipo Mungu anaweza kuja ndani yangu. Lakini ilimradi ninavitu vyangu mwenyewe Mungu hawezi kuingia ndani yangu.

Hivyo, hivyo ndivyo tunavyomtupilia nje. Tunamsukumia mbali…kutoka kwenye umaskini wetu kwenda kwenye utajiri wetu. Kutoka kwenye wa chini kuwa wa juu, tunamtoa Mungu nje ya maisha yetu kutokana na ubinafsi wetu.

Kila mara ninasema, "adui yangu mkubwa ni huyu Willium Branham." Yeye ndiye anayetoka kwenye njia ya Mungu. Yeye ndiye mvivu. Yeye ndiye anayefikiri anaweza kufanya kitu Fulani mwenyewe na anapofanya ndipo anapomtoa Mungu kwenye utendaji wake. Lakini nitakapoweza kutoka kwa mtu huyu ndipo nitakapofika mahali ambapo hayupo njiani, ndipo Mungu anaweza kuja na kutawala na kufanya mambo ambayo willium Branham hawezi kutambua nini kinafanyika.

Hapo ndipo Mungu anaweza kuwatumia. Pale anapoweza kumtumia kila mmoja wenu. Anaweza kumtumia kila mtu pale tunapojitoa njiani, lakini ilimradi tunajiweka wenyewe njiani hawezi kututumia.

Mungu alisema kwa Paulo, " Uweza wangu hutimilika katika madhaifu yako. Uweza wangu hukamilika zaidi pale unapokuwa dhaifu sana. Hivyo jinsi unavyoweza kujiachilia kwake zaidi ndipo anapoweza kukutumia.jinsi unavyozidi kusahau elimu yako , unavyosahau dhehebu lako, unavyosahau mambo hayo yote na kujiachilia kwangu, ndipo ninavyoweza kukutumia zaidi.

Kwasababu umekuwa mnyonge, nitakamilisha lengo langu kwako. ***(Warumi 8:28-30)***

Mungu anaweza kufanya kitu bora zaidi kutokana na kitu kidhaifu. Hiyo ndiyo sababu. Anafanya hivyo, pale anapochagua wanafunzi wake……..

Nani angeweza kuwazia kibinadamu mwanae mwenyewe angeweza kuzaliwa kwenye zizi la ng'ombe, kwenye lundo la samadi, kwenye nyumba ya kuhifadhia ng'ombe, na alivikwa nguo zilizorambwa na watoto wa ng'ombe? Unaona, hakuja kwenye nyumba nzuri hakupita kwenye njia za kimbinguni na gwaride la malaika wakimsujudia. Lakini alichagua kristo awe mfano wetu na alimfanya awe na umbo la kibinadamu. ***( Wafilipi. 2:5-11)***

Kamwe hakumfundisha yeye shule za ulimwengu huu, lakini alimfundisha kwa nguvu za uwezo wake ili aweze kumtumikia kikamilifu yeye mwenyewe sio kwa mawazo ya mwanadamu au ya uweza wa kilimwengu, lakini kutegemea nguvu za Mungu ***( Yohana 5:19)***

Hayo ndiyo tulionayo leo; tunajitoa sana kwenye madhehebu, dhehebu linasemaje, wanasemaje kuhusu hilo, lakini ni kinyume kabisa na mapenzi ya Mungu.tunapaswa kuleta matunda ya Roho wa mungu na kutembea vile Roho anavyotuongoza. Hilo ni kweli.

Askari wa Mungu, mashujaa, inabidi wawe wadhaifu kabla ya kuwa wenye nguvu. Kutoka kwenye udhaifu wao ndipo waweze kuwa wenye nguvu sana. ***(Waebrania 11:34).***

Hapa kuna kitu cha kutia matumaini, kitu cha kututia moyo, kwamba kutoka kwenye madhaifu na ubinadamu Mungu alituchagua watu wa aina hiyo kujenga ufalme wake. kama tunaweza kufika mbinguni, kama daima tunaweza kusimama kwenye uwepo wa Mungu na kanisa lake ni vyema kusimama na kundi la watu ambao ni wadhaifu na waliokataliwa na kutupiliwa mbali na ulimwengu na kujua kwamba hawafai kitu.

Je siungeona la kigeni kwamba Mungu anatufananisha sisi na Kondoo.? ***( Yoh. 10:1-29).*** Kondoo ndiye mnyama pekee asiyeweza kujisaidia mwenyewe aliyewahi kuwepo. Hakuna kitu kisichojitosheleza na kisichoweza kujilinda kama kondoo. Sungura anaweza kukimbia; kuchakuro anaweza kurukia miti; mbwa anaweza kung’ata, sima anaweza kusaga kila kitu; farasi anaweza kupiga mateke; ndege wanaweza kuruka; lakini kondoo anasimama asiyeweza kujilinda.

Hivyo ndivyo mungu anavyotutaka sisi tuwe. tujitambue kabisa kwamba hatujitoshelezi wenyewe, kisha Mungu anamchukua huyo mtu na kuanza kujiumba mwenyewe ndani ya mtu huyo, akiifanya mikono yake ifanye yale ambayo mkono wa Mungu ungefanya, aifanye midomo yake iseme yale tu Mungu angetaka kusema kwasababu si yake ni ya Mungu.

Alianza kwa kuumba tabia yake, akianzia kwa kutumia udhaifu wako na kutengeneza ya kwake mwenyewe.

Alituweka hapa duniani. Lakini sasa tumeelimika; tumekuwa wastaarabu. Je ulishawahi kufuatilia kwenye mlolongo wa vizazi? Tukimchukua Habili, ukaja uzao wa Sethi mpaka wakati wa Nuhu, hao wote walikuwa ni wakulima wanyenyekevu sana. Lakini watoto wa Kaini wakaanza kuwa wastaarabu, mashuhuri, wasomi, watu wakuu, wajenzi, watuwenye ujuzi. Lakini upande wa Mungu ulikuwa mdhaifu na mnyenyekevu. Ndiyo maana aliwatumia. Hiyo ndio nafasi ya Mungu. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kutupata ni pale tunapokuwa wadhaifu, ndipo tunapata kitu Fulani.

Hili linatutia moyo, sababu ufalme wa Mungu umejengwa kutokana na watu wa aina hii. Na kisha unapokuwa wa aina hiyo ujue upo kwenye ufalme wake.

Jambo muhimu kwetu ni hili, sio kwamba tunaonekana wadhaifu swala hapa ni kwamba tunanguvu nyingi. Sisi ni watu wenye uwezo mkubwa ni hilo tu.swala ni kwamba tunanguvu kubwa kichwani mwetu. Hiyo ni sahihi. Tunanguvu sana kichwani mwetu. Tunajua mengi. Mungu anapenda yatoke hayo kwetu. Hiyo ni sahihi. Tunaweza kumtolea matunda lakini tunajitolea matunda yetu wenyewe. Tunapaswa kufikiri vyema hapa, ninaufahamu wa kutosha kulijua hili.

Popote unapoona unaweza , hapo rudi nyuma na ujinyenyekeze, uwe mdhaifu jione umwanadamu na hakuna ufahamu wako unaoweza kufanya chochote. Udhaifu wa kibinadamu hautatumiwa na Mungu ndipo mungu kupitia udhaifu wa kibindamu anaweza kujimimina mwenyewe ndani yako ***( Wakolosai 1:26-27),*** kisha anakutumia mwenyewe. Unakuwa tu ni chombo ( Wagalatia. 2 :19-21). Hakika. Inakubidi ujitoe mwenyewe njiani.

Musa alijifunza udhaifu wa mwanadamu vizuri sana. Alijifunza vizuri sana, mpaka Mungu alipomuita yeye, alikuwa na madhaifu sita ambayo angeweza kutokubaliana na mwito wa Mungu.ulishawahi kusoma kwenye kitabu cha kutoka sehemu ya kwanza, madhaifu sita? Ninayo hapa niweyaandika, nataka myasikilize hayo madhaifu:

Udhaifu wa kwanza ulikuwa ni kigugumizi.

Udhaifu wa pili ni kutokuwa na mamlaka

Udhaifu wa tatu ulikuwa ni kutokuwa na lugha ya kushawishi.

Udhaifu wa nne ni kutojua lugha ya ugenini ( Kimisri).

Udhaifu wa tano ulikuwa ni mafanikio na

Udhaifu wa sita ulikuwa ni mtu wa kuchukiza.

Sasa, unajilinganisha madhaifu yako naya ya kwake na uone vile wewe unavyoweza kujiona ni mdhaifu zaidi kama alivyokuwa. "Bwana mimi sio mtu mzuri. Siwezi kusema, sijui lugha ya kimisri, siwezi kurudi kule sitakiwi mimi ni mhalifu, ooh na hayo yote. Hawatanipokea. Ninakigugumizi, siwezi kuzungumza. Ninaongea taratibu sana" ona vile alivyokuwa? Hakuwa kitu, ndugu, alikuwa akipata matibabu kule porini, ndiyo, Mungu angeweza kumtumia baada ya hayo, alikuwa akimtibu. Alikuwa na madhaifu sita tofauti na alijifunza madhaifu ya ubinadamu.

Je Mungu alimhurumia Musa kutokana na madhaifu yake aliyotoa alisema" maskini mdogo Musa, kitu Fulani kimetendeka ndani yako; umetoka kwenye degree zako …. Umekuja na kutubu kwamba huchochote, huwezi kufanya kitu. Umdhaifu sana, hapana. Mungu hakumhurumia kwa hilo. Mungu hakuchukua hilo. Mungu alishamtibu hayo mapungufu yote. (***Kutoka 4:14)*** *"Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa*. Mungu hakumhurumia yeye sababu ya madhaifu yake. Unasema " Ooh Bwana, ninajisikia vibaya sana. Siamini nitaweza kufanya hili" Mungu hawezi kukuhurumia wewe kwa hilo: anajisikia kukupiga teke kidogo utoke mbele yake. Mungu hakuonei huruma wewe. Anashikwa na hasira juu yako. Unaendea umbo ambalo yeye anaweza kukutumia wewe.

Kama Paulo alisema, yeye alikuwa haoni vizuri, kitu Fulani kilikuwa kinamsumbua sana. Shetani anamyumbisha yeye huku na huko. Na akaenda kumuona Bwana. Mara tatu, aweze kuyatoa hayo kwake, alisema, " Sipendi hili, Bwana, ondoa hili mbali na mimi"
***(I Wakorintho 12: 1-10)*** na kisha usiku mmoja Bwana akasema naye, Paulo neema yangu yakutosha.

Akasema, “*Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi.* Nitayafurahia hayo. Ninajua wewe ndiye mponyaji. Nimeona ukiponya wagonjwa, ukifufua wafu, ukitoa pepo, ukifungua macho ya vipofu wakaona, basi kama nimekujia wewe na unaniambia kwamba neema yako yanitosha, ndipo sasa, huyu ibilisi anayenisumbua mimi ni kukua kwa maumivu ya neema. ndipo nitayafurahia madhaifu yangu” kwanini? “Ni afadhali nipate kiwango cha juu cha ufunuo mkuu unaotoka juu.”

Unaona, alikuwa Na kitu Fulani ambacho mitume wengine hawakuwa nacho. Alimuona yeye alipokuwa akifa, akizikwa, akifufuka na akipaa juu. Alimuona yeye. Miongoni mwao walisema, “Vyema nilitembea na yeye” hilo lilifanywa na kila mtu mtaani. Lakini baada ya yeye kufa, kuzikwa, na kufufuka na kupaa juu na kurudi tena kwa umbo la nguzo ya moto, alisema na Paulo.hilo lilikuwa bora kuliko wote waliotembea naye. Amina.

Yeye alisema, “kama inanibidi nipandishwe cheo ili niweze kujenga seminari kubwa, ni afadhali niwe wa chini na nipate kiwango cha juu cha ufunuo huu mkubwa wa kutoka juu, Mungu anamuacha mjumbe wa ibilisi anipige teke chini” yeye anasema, ndipo sasa pale ninapojiona mdhaifu ndipo ninapokuwa na nguvu.Amina amina. Kukuwa kwa maimivu ya Neema!. Amina tunaweza tukakaa hapa na hili kwa muda mrefu sana; tunauguzwa na maimivu ya Neema yake.

Oooh, ataruhusu njia za mkato kutujaribu, ili aweze kutukamilisha kwa kazi yake. Anaweza kuruhusu hilo sasa, kanisa ataruhusu njia za mikato kwaajili ya huduma zetu

## Nukuu ya kingereza:

[1] “nguvu kamilifu kutoka kwenye udhaifu mkamilifu” ( 61-1119), par. 42-62, 89-100, 111-123, 166-169, 181-183. [2] “Shalom” (64-0112), par217-222)

---

Jiwe la kiroho la kujengea Na. 31 (Mpya 2014) kutoka neno lililofunuliwa la wakati huu,
Imeunganishwa na: Gern Rodewald, Friedenstr. 69, D-75328 Schomberg, Germany.
www.biblebelievers.de, Fax: (+49) 72353306

---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia.
Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk724.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*